


# Huru kwa ajili ya kupenda



Mahali walipo masista wa Antonia Maria Verna ulimwenguni. Maisha yaliyoelezwa kupitia vibonzo ni ya Antonia Maria Verna. Historia fupi na ya kina ni ya mwanamke aliyelewa kwamba elimu na utamaduni ni misingi dhidi ya ukandamizwaji. Alipambana vikali kwa imani thabiti dhidi ya umasikini wa kimwili na kimaadili. Imani imara katika Bikira Maria Mkingiwa dhambi ya asili, Mama wa Yesu na Mama yetu aliye chemchemi isiyokauka ya neema na matumaini. Ni mang'amuzi ya maisha ya sasa ya mwanamke ambaye hakuogopa kupenda.

# Huru kwa ajili ya kupenda

Maisha ya Antonia Maria Verna  
Mwanzilishi wa Masista wa Upendo  
wa Bikira Maria Mkingiwa dhambi ya asili wa Ivrea



 TAV editrice

# Huru kwa ajili ya kupenda

Maisha ya Antonia Maria Verna

Mwanzilishi wa Masista wa Upendo  
wa Bikira Maria Mkingiwa dhambi ya asili wa Ivrea



# Huru kwa ajili ya kupenda

Mpango

Mwanzilishi wa Masista wa Upendo wa Bikira Maria Mkingiwa dhambi ya asili wa Ivrea  
Lapislunae - Tau Editrice

Maandishi

Luigi Mezzadri

Storyboard

Giuliano Rossi

Michoro

Andrea Lucci

Rangi

Antonio Scricco

Kimetafsiriwa na

SCIC

© TAU Editrice

Via Umbria 148/7

06059 Todi (PG)

Tel. +39 075 8980433

[www.editricetau.com](http://www.editricetau.com)

[info@editricetau.com](mailto:info@editricetau.com)

ISBN 978-88-6244-170-4

Haki zote zimehifadhiwa

Kimechapishwa katika mwezi wa Septemba, 2011

## PRESENTAZIONE

Hii ni historia ya mwanamke, mtoto wa mkulima, Mwenye heri Antonia Maria Verna ambaye, tangu utoto, alitambua wito wa pekee kutoka kwa Bwana kwa ajili ya utume wa upendo: yaani kuwaelimisha watoto kwa kuwafundisha, katekesimu (licha ya katekisimu), kusoma na kuandika katika nyakati ambapo elimu ilidhaniwa kuwa ni kwa ajili ya matajiri tu, kuwatunza wazee na wagonjwa hata katika nyumba zao; akitoa kipaumbele kwa maskini zaidi na, kama alivyopenda kusema yeye katika unyofu wake, daima “bure”.

Antonia Maria Verna alianza utume wake akiwa mdogo sana, wakati alipokuwa akifanya mafundisho ya katekisimu kwa ajili ya kupokea komunyo ya kwanza. Aliporudi nyumbani aliwakusanya watoto wenzake majirani na kuwafundisha yale aliyokuwa amejifunza; pia alianzisha kashule kadogo, alijitafutia muda wa kujitoa kwa ajili ya wagonjwa na hivyo akajipatia upendo na heshima kwa watu wote majirani.

Aliacha familia yake na aliamia Rivarolo, akiwa mwaminifu katika nadhiri ya useja aliyokuwa ameiweka mbele ya Bikira Maria Mkingiwa dhambi ya asili wakati alipokuwa na miaka 15 na alidhihirisha wazi wito wake wa upendo. Kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya utume wake alikwenda kijiji cha karibu, akisafiri kilomita 12 kila siku kwa ajili ya kujiendeleza.

Wakati huo alikuwa na umri wa miaka 30.

Antonia Maria alikuwa na uhakika kwamba kumkomboa mwanadamu kutoka ujinga maana yake ni kumrudishia mtu heshima na matumaini kwa maisha yaliyosimikwa juu ya fadhila za kiutu na kikristo

Matatizo hayakukosekana katika utume alioanzisha bila kuwa na vitega uchumi, akijikabidhi katika Maongozi ya Mungu na ukarimu wa watu mahalia; kwa kufanya hivyo alikuwa na uhakika kwamba hiyo ndiyo njia ambayo Mungu amemwitia kufuata; akiimarishwa na imani thabiti alipata nguvu ya kuendelea mbele na kushinda vipingamizi katika sala.

Vibonzo hivi vilivyoandikwa katika lugha ya kiitaliano, kihispania, kiingereza na kiswahili, vinawakilisha kwa kifupi sehemu muhimu za tukio hili la upen-

do lisilo la kawaida kwa mtindo rahisi, zikisaidiwa na michoro maalum, vikiwa na uwezo wa kuvuta hisia za vijana wengi.

Mazungumzo, mafupi na ya kina kati ya wahusika katika masimulizi, yanaonyesha mwangaza alioangaziwa Mama Antonia, moyo wake wazi, karama yake, maisha yake ya kiroho, uimara na udumifu katika kuendelea mpaka mwisho, kujitoa kwake bila kujibakiza kwa unyofu na upendo, uwezo wake wa kuwa kama punje ya ngano iliyosagwa na kuwa mkate ... katika hostia nyeupe kama Bikira Maria Mkingiwa dhambi ya asili.

Michoro inatoa mvuto wa ndani, iko wazi, inagusa mioyo ya wasomaji, hata mpangilio wake na rangi unaleta uwiano unaotoa mguso wa pekee kwa wasomaji wake.

Maandishi yametayarishwa na padre Luigi Mezzadri.

Michoro ni ya Andrea Lucci.

Tukisoma vibonzo hivyo tunapata hamu ya kutangaza kwa jamii maisha ya pekee ya Mwenyeheri Antonia Maria Verna, na kufufua katika mioyo ya vijana wengi hamu ya kufuata mfano wake angavu.

Angelo Montonati

# Huru kwa ajiũ ya kupenda

Huko Rivarolo Canavese, kwenye mji mzuri na wa zamani, chini ya milima, kuna Kanisa ambalo limejengwa pale alipopita Mt. Francisco aliyeishi kitakatifu na katika hali ya kimaskini.



Wakati Mt. Francisco alipotembelea mahali pale, aliacha kumbukumbu ya faraja kwa watu, hasa maskini...



Upendo wake kwa watu, huko Rivarolo, uliendelezwa na mapadre wake. Mbele ya conventi yao kulikuwa na msururu wa maskini kila siku...



Alizaliwa Pasquaro, karibu  
na Rivarolo, katika mkoa wa  
Torino, tarehe 12 Juni 1773,  
kutoka familia ya  
kimaskini sana



Wakati alipozaliwa aliwaletea wote  
mng'ao wa furaha



Mmenawa mikono?  
Antonia uwe mwangalifu na  
kaka yako huyo  
mtundu sana"



Nyumba ilikuwa ndogo, lakini ushirikiano  
ulikuwa mkubwa sana. Walipungukiwa  
vitu vingi, lakini upendo haukukosekana



Antonia alikuwa mwema  
na mtii. Alikuwa amejifunza  
kusali mbele ya sanamu  
ya Bikira Maria iliyokuwa  
nyumbani







Wakati wa mafundisho ya katekismu alikuwa msikivu sana

Angalia, Antonia anajifanya mtakatifu. Anataka kujionyesha!!!



Wakati aliporudi nyumbani alikusanya watoto na kuwafundisha katekismu..

Yohane: "Mungu ni nani?"

Mungu ni Upendo



Nilikuwa nimemwuliza Yohane, lakini nafurahi kwamba mmejifunza vizuri wote




Mama yangu amefariki. Sasa yuko wapi?

Yuko mbinguni



Antonia, ni kweli kwamba watakatifu wanaenda mbinguni?

Ndiyo, ni kweli




Kwa hiyo nitakwenda pamoja nawe mbinguni?

Ndugu zake wangependa kumtafutia mchumba, hata kwa sababu alikuwa mzuri




Nitakapokuwa mkubwa ningependa kuwa na watoto

Wangapi?



Lakini hamu ya Antonia Maria ilikuwa tofauti. Hakuwa kinyume na ndoa, ambayo ni sakramenti... lakini alikuwa anajisikia wito wa kuwa huru na vifungo vyovyote.

watano au... sita



Mimi zaidi... lakini siyo wa kwangu... nataka kuwa na watoto wengi wa kuwafundisha katekismu, kucheza nao na kuwa mwalimu wao... watoto wasiojua kusoma na kuandika watakapokuwa wakubwa watatendewa kama watumwa maskini, mimi sipendi hayo...



Licha ya kuwa na rafiki zake, Antonia, alijenga urafiki wa pekee na wa kudumu na Bikira Maria...

Bikira Maria, napenda sana kutolea maisha yangu kwa ajili ya kumtumikia Mungu na watu... Niambie nifanye nini...

Alikuwa anasikia kwamba Mungu anataka kitu zaidi kutoka kwake.



Kwa hiyo Antonia, kwa ukarimu na furaha, akiwa na miaka 15, aliweka nadhiri ya kubaki bikira. Alitoa maisha yake kwa Bwana kwa nia ya kupambana na ujinga na maskini, kwa sababu aliamini kwamba inawezekana kubadili hali ya maisha...

Yeye alifanya utume kwa bidii na amari alishirikisha imani yake kwa moyo



Alikuwa na maneno mazuri kwa wote. Siku moja maskini alimwomba msaada



Akisukumwa na hitaji la kuwa huru ili kujitoa kwa ajili ya wengine, aliamua kuishi peke yake. Rafiki yake mmoja alimwambia:



Aliwapokea wasichana waliopenda kushiriki maisha ya utume, yaani kujitoa kwa ajili ya wengine



Kwa maandalizi zaidi, Antonia alirudi  
kwenye madawati ya shule



Kila siku alikuwa akitembea  
km 12 kwa miguu



Hata kama kulikuwa na barafu yeye  
hakukosa kwenda shuleni




Matatizo hayakukosekana

Tunawezaje kufanya shule bila hata senti moja?

Tusiogope. Maongozi ya Mungu na Mt. Yosefu vitatusaidia



Tungepaswa kutoza, walao kidogo




Bikira Maria Mkingiwa dhambi ya asili alipokea yote bure na akatoa yote bure.




Alijachia kwa matumaini kama mtoto mikononi mwa mama yake




Ametoa  
«YOTE BURE»









Mnaonaje kama tutajenga jumuiya  
kama ile ya Cuceglio, ya masista wa  
Kupashwa Habari?



Jumuiya ndiyo, lakini iliyo  
wazi kwa mahitaji ya watu, kwa  
wagonjwa, maskini, yatima, wasichana  
wanaohitaji elimu na malezi ya  
kikristo... jumuiya iliyo chini ya ulinzi wa  
Bikira Maria Mkingiwa dhambi ya asili,  
yenye moyo mpana  
kama moyo wake



...tutaishi pamoja kama masista, tuki-  
mweka Yesu kama kiini cha maisha yetu.  
Yeye atatusaidia kupendana na kuwasai-  
dia wote wenye shida. Wapi, bado hatuju-  
wi, tutatafuta nyumba.  
Hatutatafuta cheo, isipokuwa kuishi  
upendo, unyofu na unyenyekevu

Mnaliona waridi hili? Ni zuri kwa asili yake. Hata  
na sisi. Mimi nilikuwa wa mwisho kwenye kijiji  
changu. Nani angeweza kufikiri kwamba Mungu  
angenichagua mimi? Ningeweza kusema hapana?  
Vivyo hivyo hata wewe hata ninyi ni wazuri kama  
waridi hili. Twendeni, tumtumikie Mungu



Tarehe 10 juni 1828 ilikuwa siku iliyoangazawa na jua



Tumeacha wazazi wetu, nyumba zetu, watoto ambao tungewapata, ili tuwe huru kwa ajili ya kumtumikia Bwana. Tumesubiri sana na... mwisho! Leo tarehe 10 juni 1828 tunaweka nadhiri zetu za useja, ufukara na utii, ambazo zitatuweka huru kwa ajili ya Mungu na watu

Jumuiya ilianza kwa miujiza mingi midogo midogo, lakini ya upendo wa kweli



Mara nyingi ili kuwapa maskini mkate walibakiwa na kabati tupu



Maongozi ya Mungu yanawalinda



Mkate huu na maziwa ni kwa ajili yenu

Marianna, tumshukuru Mungu pamoja nawe, kwa sababu leo hatukuwa na chochote kabisa cha kula

Wakati wa vuli baada ya mavuno alileta




kiasi cha maboga, maharagwe, viazi na unga...

Bwana akubariki wewe na familia yako kwa ukarimu, tutatenga kiasi kwa ajili ya maskini!

Kama ilivyo mara kwa mara kwenye kazi ya Mungu, baada ya jua, radi inafuatia



Peke yetu hatuwezi ... tumepata nyumba, lakini bado ni ya kumaliza malipo, tuna uhusiano mzuri na masista wa Montanaro, kwa nini hatuungani nao moja kwa moja?



Wasichana wengine wanajunga na Mama Antonia, kundi linaongezeka; wanaanza utume hospitalini. Padre Durando, mtu wa Mungu, kijana na mkali kidogo alitoa mchango mkubwa wa ukuaji wa Shirika, lakini aliwalazimisha Mama Antonia na wenzake kujiunga na Masista wa Montanaro na Mabinti wa Upendo wa Ufaransa



Wanataka tuvae kifaransa, ni kweli Mabinti wa Upendo ni wengi, wamejipanga vizuri, wana Mwongozo wa maisha, lakini kujiunga nao ni kama kukana utambulisho wetu ambao msingi wake ni katika fumbo la Bikira Maria Mkingiwa dhambi ya asili. Hatutaweza tena kwenda usiku kwa wagonjwa. Mwongozo wao hauruhusu masista kutoka usiku






"Tunawezaje kuwa tayari kwa wote, matajiri na maskini katika kuelimisha na kufundisha katekismu? Kujionga na Mabinti wa Upendo ingekuwa nafuu, tusingejihatarisha lakini, tungalit mpango ambao Mungu ametukabidhi"






Nani amewaambia kwamba hatuwezi kubadili kitu hata kama tu kundi dogo? Kwa nini mnaogopa kuwa huru? Jumuiya zote huzaliwa ndogo, kisha hukua..



Ni kweli tupo wachache, tu wanawake, thamani yetu ni ndogo katika jamii, tu maskini na dhaifu, lakini ndani yetu kuna nguvu ya Mungu na hilo linatutosha kwa ajili ya kukabiliana na magumu.




Tazameni Bikira Maria: Baba wa mbinguni alimkabidhi Mwanaye Yesu. YEYE ALIKUWA MWANAMKE. kama mimi, kama wewe, kama sisi.

Masista wake wengi walikwenda kwa Mabinti wa Upendo



wanabaki kutazamana





Tazameni hizi punje za ngano.  
Ni ndogo, hazina mtetezi,  
kama sisi...



Lakini ziko HURU.  
Ziwekeni udongoni,  
zitakuwa masuke. wakati  
masuke yatakusanywa,  
yatasagwa na kuumu-  
shwa katika maji yataku-  
wa mkate... zaidi...



Yanaweza kuwa HOSTIA,  
...nyeupe kama Bikira Maria  
Mkingiwa dhambi ya asili...  
tunataka kuwa hivi hata sisi?...

Ndiyo,  
tunapenda...



# ...tunataka kuwa huru kwa ajili ya kumtumikia mungu na watu

Antonia Maria Verna  
aliaga dunia huko Rivarolo Canavese  
siku ya Noeli mwaka 1838  
akifurahi kwa sababu alifungua njia ya uhuru  
kwa wanawake waliopenda kujitoa kwa mungu  
bila kujibakiza kwa kuishi upendo upeo





Antonia Maria Verna,  
Dada wa upendo  
aliye huru katika kusema ndiyo kwa  
Bwana kwa ajili ya utumishi wa ndugu.  
Ametangazwa na Kanisa kuwa  
Mwenyeheri tarehe  
2 Oktoba 2011,  
katika Kanisa Kuu la  
Bikira Maria Aliyepalizwa mbinguni,  
jimboni Ivrea.  
Maisha yake yanatuangazia pia sisi,  
yanatufungulia upeo wa matumaini,  
yanatufariji katika kuwa huru kwa  
ajili ya kumpenda na  
kumtumikia Mungu na watu.

# Safari endelevu...

Upendo ulio wazi na usio na mipaka wa Mama Antonia ulipata mwendelezo katika safari ya masista, ambao, kama yeye, wamejitahidi kukidhi mahitaji ya watu.



Masista wanaendelea kuwa kama punje ya ngano iliyopandwa katika ardhi ya Kanisa kwa ajili ya kuwa masuke ya ngano na baadaye hostia pamoja na Yesu kwa ajili ya kulisha watoto, vijana, familia, wazee, wagonjwa, maskini na wote wenye kuhitaji. Huu ni wajibu na urithi wetu, kama wafuasi wa Mama Antonia Warithi wa upendo wa Mama Antonia tunaendelea kwa ujasiri katika safari ya kujitoa bila kujibakiza.





Bikira Maria Mkingiwa dhambi ya asili ambaye alisema ndiyo bila masharti, anatumfundisha kutokuwa na mipaka katika utume wetu; kwa sababu hiyo kuanzia masista wetu wa mwanzo tumefunga safari ya umisionari kuelekea mashariki: yaani Uturuki, Lebanoni, Israeli tukishiriki utamaduni na kuheshimu imani tofauti za watu, kwasababu upendo ni amri ya Yesu, na pia tumeelekea Libia, Argentina, Pennsylvania, Tanzania, Kenya na mwisho Albania na Mexico kwa ajili ya kupeleka Injili ya matumaini na furaha hata katika Msalaba.

Chama cha Wamisionari wa Upendo, waliojitoa kwa Bwana kwa kuishi mashauri ya kiinjili katika nadhiri za ufukara, useja na utii na walei Waverniani, wanashiriki karama, roho na utume wa shirika letu, ambao katika familia na jamii, wanajitahidi kuwa chachu ya kiinjili ya upendo, unyofu na unyenyekevu wa Mama Antonia Maria Verna. Anayewaangazia safari yao ni Bikira Maria Mkingiwa dhambi ya asili, aliye huru katika kujitoa kwa upendo wa bure, aliyezungukwa na uzuri wa Mungu anayekomboa ulimwengu. Tunapenda kuwa huru na wazuri pamoja naye?  
Tuanze safari...  
Hata sisi.....  
Hata wewe.....



# Watoto wanamwandikia Mama Antonia

Mama Antonia,  
wewe uliwafundisha  
watoto maskini  
ambao hawakuwa na uwezo  
wa kwenda shuleni kusoma  
na kuandika,  
ulisaidia familia maskini.  
Unaendelea kutupenda  
na unatusaidia hata sisi  
ili tuweze kupendana.

Marilena  
Shule ya Carmine, Bari

Andika hapa shairi lako juu  
ya Mama Antonia



Andika hapa maoni yako juu ya  
Mama Antonia





Andika hapa barua yako kwa  
Mama Antonia

## KWA MAMA ANTONIA

Nilijua jina lako tu,  
niliposoma maisha yako  
ya kwangu, ambayo nilifikiri  
yalikuwa angavu,  
yameonekana tu  
kama mchoro wa penseli.

Ndiyo,  
Maisha yako ni mazuri zaidi,  
bahati yako!  
Utotoni hukuwa mtundu,  
bali kwa Yesu ulikuwa binti  
mpendwa.

Sasa nahisi uko karibu nami  
Moyoni nitabaki nawe daima.

Unajua kwa nini?

Kama watoto wengine hata mimi ni  
mtoto,


Ambao wewe umewapenda daima.

Federica Infante  
Umri: miaka 10  
Gorga (Salerno)





# Uwepo wa Masista wa Mwenyeheri Mama Antonia Maria Verna ulimwenguni



Tukiangazwa na fumbo la Bikira Maria Mkingiwa Dhambi ya asili, Masista wa Mama Antonia tunaishi Roho ya kujitoa bila kujibakiza kwa maskini zaidi katika nchi 11 ulimwenguni.

- Italia tunafanya utume mashuleni, parokiani na katika shughuli nyingi za kijamii,
- Albania tunafanya kazi na watu vijijini na parokiani.
- Uturuki tunashiriki katika malezi ya watoto na vijana, tukiheshimu sana tofauti za dini mbalimbali.
- Lebanoni tunafanya kazi mashuleni tukijitoa bure kwa wote.
- Israeli tunashughulika katika kutoa elimu kwa watoto kwa manufaa ya familia za Kikristo na kiislamu.
- Libya tunahudumia wagonjwa.
- Tanzania na Kenya tunafanya utume mashuleni , mahospitalini, tunatoa huduma kwa watu vijijini na parokiani
- Argentina tunafundisha mashuleni, tunawajibika katika utume wa uinjilishaji na utoaji wa huduma kwenye makazi duni.
- Mexico tunafanya utume wa uinjilishaji.
- Pennsylvania tunatoa huduma ya elimu kwa mtindo wa Montessori

Safari inaendelea .... Kwa kujitoa bure

## Suore di Carità dell'Immacolata Concezione d'Ivrea

Via della Renella, 85

Tel. +39 06 5818145 - Fax +39 06 5818319

00153 ROMA

[www.scicivrea.it](http://www.scicivrea.it) - [vernanelmondo@scicivrea.it](mailto:vernanelmondo@scicivrea.it)